# MATUMIZI YA ISTILAHI KATIKA KISWAHILI NA JINSI YANAVYOATHIRI MAWASILIANO

*J.S. Mdee*

## 1.0 Utangulizi

Lugha yoyote hufanikisha mawasiliano miongoni mwa wazungumzaji wake iwapo kila mzungumzaji anafahamu msamiati unaotumika. Mawasiliano huathirika itokeapo baadhi ya wanajamii hawaelewi maana ya msamiati unaotumiwa katika mazungumzo. Mawasiliano yanapotumia lugha ya kitaalamu huathirika pia iwapo istilahi zinazotumika hazifahamiki kwa wazungumzaji wote. Istilahi ni msamiati maalumu unaotumika katika mawasiliano miongoni mwa wanasayansi wa fani mahsusi. Istilahi huunda lugha ya fani maalum ya sayansi ambayo wataalamu wake huielewa. Ili watu wapate kuielewa lugha ya sayansi hawana budi kujifunza msamiati wake na asiyeujua msamiati huo hatoelewa kinachozungumzwa.

Istilahi za fani moja ya sayansi ni jumla ya msamiati wote unaotumiwa katika fani hiyo na wanasayansi wanaohusika. Kwa mujibu wa makala hii, fani za sayansi hujumuisha sayansi za jamii, k.v jiografia, isimu, uchumi; sayansi za asili, k.v. biolojia, zuolojia, jiolojia; na sayansi matumizi k.v. fizikia, uhandisi, eletroniki, kompyuta, n.k. Kila moja ya nyanja hizi za sayansi ina msamiati wake ambao huunda lugha ya kitaalamu ya sayansi hizo.

Istilahi huundwa ili kuwakilisha dhana ngeni ambazo hazina maneno ya kuziwakilisha katika lugha. Dhana mpya za kisayansi huweza kugunduliwa na wanajamii wenyewe kutokana na uchunguzi wanaoufanya au huweza kuingia kutoka lugha za jamii zilizoendelea kisayansi na kiteknolojia. Dhana mpya inapoingia katika lugha huhitaji neno la kuiwakilisha, ambalo ama ni neno lililopo katika lugha yenyewe au ni neno jipya linaloundwa maalum kwa dhana inayohusika. Uundaji wa istilahi ni ishara ya kukua kwa lugha kwani kunaifanya lugha kuwa ya kisasa na huipa uwezo wa kueleza dhana za fani mbalimbali ambazo mpaka wakati huo zilikuwa hazielezeki kwa lugha hiyo, ila kwa lugha zilizoendelea peke yake. Kutokana na hali hii ni dhahiri kuwa istilahi huvunja vikwazo vya mawasiliano (Mukuthuria 2000) na husaidia kufanikisha mawasiliano miongoni mwa wanajamii wa taaluma husika, na kurahisisha kuenea kwa maarifa katika jamii (Mwansoko 1995). Lakini ili mawasiliano yakamilike ni lazima watumiaji wake wote waufahamu msamiati huo.

Matumizi ya msamiati na istilahi zisizosanifiwa au kufahamika huathiri ufanisi wa mawasiliano kwa wanajamii au miongoni mwa wazungumzaji au wataalamu wa somo ambapo istilahi hizo hutumika. Katika makala hii tutajadili jinsi istilahi zinavyoweza kuathiri mawasiliano, mambo yanayosababisha kuwepo kwa hali hii, na mapendekezo ya kuirekebisha. Kabla ya kufanya hivyo hebu kwanza tuchambue aina za istilahi.

## 2.0 Aina za Istilahi

Istilahi zinaweza kugawanywa katika makundi mawili kulingana na aina ya sayansi inayowakilishwa: istilahi za sayansi menyu na istilahi za sayansi pendwa. Istilahi za sayansi menyu ni msamiati wa sayansi ambao ni mahsusi kwa wanataaluma wa fani hiyo na hufahamika kwa wanataaluma wa fani hiyo tu. Mfano wa istilahi hizi ni kama zile za isimu, fasihi, leksokgrafia, fizikia, kemia n.k. Istilahi za leksikografia kama vile kidahizo, kitomeo, lugha kienzo, wimbi n.k. na istilahi za fasihi kama vile jazanda, balagha, maleba, fanani n.k. au istilahi za isimu kama vile kishirikishi, kirai, sentensi sahili, ngeli, yambwa au kishazi ni mahsusi kwa fani zinazohusika na hazifahamiki wala kutumika nje ya mazingira hayo wala katika lugha ya kawaida.

Istilahi za sayansi pendwa ni msamiati wa sayansi iliyovuka mipaka ya kuwa miliki ya wanasayansi peke yao na kuenea hadi kwa walei, yaani watu wasio wa fani hiyo hata ikaingia kwenye lugha ya kawaida. Sayansi pendwa ni maarifa ambayo yameingizwa katika jamii ili yatumike kwa manufaa ya jamii. Sayansi pendwa hujumuisha elimu ya afya, tiba, mazingira, uchumi, lishe n.k. Maarifa haya huenezwa kwa njia ya mihadhara, hotuba, mafunzo, vitabu, na vyombo vya habari kama vile redio, televisheni au magazeti. Kwa mfano, elimu ya afya kuhusu virusi au bakteria wenye kusababisha au kueneza maradhi mbalimbali, kinga na tiba ya maradhi ambayo tunaipata katika hospitali, semina au kujisomea kutoka katika vitabu au majarida ni sayansi pendwa. Awali maarifa haya yalipokuwa yanatafitiwa na kufanyiwa majaribio na wanasayansi wa elimu ya virusi (virusiolojia) katika maabara yalikuwa ni sayansi menyu kwa kuwa ilikuwa mahsusi kwa wanasayansi wa virusiolojia. Lakini baada ya uchunguzi kukamilika na matokeo ya utafiti kusambazwa kwa jamii ambayo sio ya wataalam ili wayafahamu maarifa haya na kuyatumia, sayansi hii huacha kuwa menyu na badala yake huwa sayansi pendwa.

Istilahi za sayansi pendwa na sayansi menyu huundwa na kutumika katika kila lugha ya jamii inayoendelea. Katika jamii ambayo lugha yao ndio pia lugha ya elimu, msamiati wa sayansi pendwa huingia katika lugha na kuwa msamiati wa kawaida kwa kuwa huupata kupitia elimu wanayofundishwa shuleni au kwa kujisomea vitabuni. Katika jamii ambapo lugha ya jamii sio lugha ya elimu, lugha yao haitokuwa na msamiati wa sayansi pendwa. Kwa hali hii istilahi za aina hii ya sayansi zitapaswa kuundwa ili kueneza sayansi pendwa kwa jamii. Linganisha maneno ya Kiingereza: *webpage, e-mail, internet* n.k. ambayo yamebuniwa zama hizi za Sayansi na Teknolojia huko Ulaya na tayari yameenea huko kama sehemu ya msamiati wa sayansi pendwa na kuingia katika lugha ya kawaida. Msamiati huu haujaingia katika Kiswahili na kwa hali hiyo haujaundiwa istilahi. Sasa hebu tutazame jinsi istilahi zinavyotumiwa.

## 3.0 Matumizi ya Istilahi

Istilahi hutumiwa na wataalamu wa fani mbalimbali kuandika vitabu au makala katika fani zao ili kuelimisha jamii. Wahadhiri nao hutumia istilahi wanapofundisha dhana anuwai

katika nyanja zao. Halikadhalika waandishi wa habari na wafasiri huandika makala katika magazeti, hufasiri vitabu au makala wakitumia istilahi kueleza dhana katika lugha ya kitaalamu. Iwapo lugha lengwa ni ya kufundishia katika kiwango chochote cha elimu, vitabu vya kufundishia huandikwa au kutafsiriwa kwa kutumia istilahi za fani zinazohusika. Kutokana na hali hii, maarifa mbalimbali ambayo awali yalikuwa katika lugha ya kigeni, hufundishwa au kusomwa katika lugha ya jamii ambayo hadi wakati huo ilikuwa ni lugha ya mawasiliano ya kawaida tu. Kwa kuwa maarifa mengi yaliyo katika lugha za jamii zilizoendelea ni mageni katika lugha za jamii zinazoendelea, istilahi mpya huifanya lugha kuwa mpya na ngumu kwa wazungumzaji wake kwa vile istilahi ni msamiati mgeni unaoeleza dhana ngeni kwao.

## 4.0 Matumizi ya istilahi katika Kiswahili

Uundaji na utumiaji wa istilahi mpya katika Kiswahili unachangia katika kuikuza lugha na kuifanya iwe ya kisasa. Maendeleo haya yanawawezesha Waswahili kupata maarifa ya kisasa katika lugha yao. Nchini Tanzania kwa mfano, Kiswahili kimekuwa lugha ya kufundishia elimu katika Shule za Msingi na Vyuo vya Ualimu. Kwa zaidi ya miaka 30 Kiswahili kimekuwa kikifundishia somo la isimu na fasihi katika shule za sekondari na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kuanzia wakati huo istilahi za masomo hayo ziliandaliwa na kutumika. Huko Kenya Kiswahili hufundishia isimu na fasihi katika vyuo vikuu ambapo tasnifu za uzamili katika fani hizi zimekuwa zikiandikwa kwa Kiswahili pia. Kiswahili kimeendelea pia kutumiwa na wanasiasa, waganga na watendaji wa serikali katika kueleza umma masuala ya siasa, uchumi, afya, lishe na mazingira ambayo ni mageni pia katika lugha hii. Vyombo vya habari navyo hutumiwa pia kuelimisha jamii kuhusu masuala hayo na hutumia istilahi za Kiswahili. Istilahi kama msámiati wa kisayansi ni maneno mapya na mageni kwa wazungumzaji ambao ni walei katika fani hizo. Kutumika kwa istilahi hizi kwa wasio wa fani inayohusika, huwatatiza wasielewe kinachosemwa.

Kiswahili kama lugha inayoendelea haina msamati wa sayansi pendwa kwa vile nayo ni maarifa mapya ambayo yanafikishwa huku kwetu kupitia lugha za kigeni. Kwa hivyo msamati wa sayansi pendwa huku bado ni istilahi ambazo hazina budi kuundwa na kutumiwa ili kuieneza sayansi pendwa kwa watu wetu ambao hawaijui na lugha yake hawaifahamu pia. Istilahi hizi zikishaundwa hazina budi kutumika japokuwa hazifahamiki. Hapana shaka kuwa istilahi zinapotumika kwa mara ya kwanza huwatatiza wasomi au wasikilizaji, lakini kadiri istilahi zinavyotumika, huzoeleka na kufahamika kwa wazungumzaji wa lugha ile na kuwa msamiati wa kawaida. Hebu sasa tuchunguze mambo yanayosababisha matumizi ya istilahi kuathiri mawasiliano.

## 5.0 Usuli wa istilahi kuathiri mawasiliano

Wataalamu mbalimbali wa sayansi menyu wanapotaka kutumia Kiswahili kama lugha ya mawasiliano hukabiliwa na tatizo la ukosefu wa istilahi za Kiswahili kwa fani zao.

Kutokana hali hiyo, hulazimika kuunda istilahi kwa matumizi yao. Mfano wa juhudi hizi ni uundaji wa istilahi za kufundishia isimu ya Kiswahili katika vyuo vikuu vya Dar es Salaam, Kenyatta, Nairobi na Moi. Wanaisimu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam waliandaa na kutumia istilahi za isimu na baadhi ya istilahi hizo zimechapwa katika Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha. Baadhi ya wanaisimu wa Chuo Kikuu cha Moi wamebuni na kutumia stilahi za isimu kwa dhana ambazo wanaisimu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam tayari wameunda istilahi kama mfano katika jedwali la 1 unavyoonyesha.

**Jedwali la 1: Istilahi za isimu ya Kiswahili**

| Istilahi za Kiingereza | Istilahi za Kiswahili za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam | Istilahi za Kiswahili za Chuo Kikuu cha Moi |
|---|---|---|
| *vocal cords* | nyuzi za sauti | nyuzi za glota |
| *vocal tract* | mkondo sauti | bomba la sauti |
| *gender* | jinsia | uana |
| *nasal* | nazali | ung'ong'o |
| *source language* | lugha chasili | lugha changizi |

Kwa kuwa istilahi za isimu na lugha zilizoandaliwa Dar es Salaam zilifahamika kwa wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Moi, ni dhahiri kuwa istilahi za Dar es Salaam hazikukubalika kwa wanaisimu wa Moi. Hii ndio maana wakaunda zao. Kutokuwa na istilahi sanifu za Kiswahili kwa isimu na lugha zinazokubalika kwa watumiaji wake wote, huathiri mawasiliano miongoni mwa wanaisimu wa Kiswahili wa Afrika ya Mashariki kwani wanakosa lugha moja inayowaunganisha, lugha itakayofanikisha mawasiliano miongoni mwao. Makala iliyoandikwa na mwanaisimu wa Chuo Kikuu cha Moi yenye *nyuzi za glota, bomba la sauti na ung'ong'o* itamtatiza mwanaisimu asiyezijua na ambaye anatumia istilahi nyingine.

Hali hii ya kuwa na istilahi zaidi ya moja kwa dhana moja hujitokeza kwa kazi za watu binafsi pia. Tazama mfano 2 kuhusu istilahi za Kihore na wenzake (1999) na zile zinazotumiwa na Khamisi na Kiango (mswada) kwa dhana zilezile:

**Jedwali la 2: Istilahi za sarufi ya Kiswahili**

| Istilahi za Kiingereza | Istilahi za Kihore na Wenzake, (1999) | Istilahi za Khamisi na Kiango (mswada) |
|---|---|---|
| *prepositional phrase* | kirai-kiunganishi | kirai husishi |
| *adjectival phrase* | kirai-kivumishi | kirai vumishi |
| *verbal phrase* | kirai kitenzi | kirai tenzi |

Msingi wa tofauti ya Kihore na wenzake kwa upande mmoja na Khamisi na Kiango kwa upande mwingine unatokana na mtazamo wao wa kuainisha kategoria za maneno katika Kiswahili. Kihore wanaamini kuwa Kiswahili hakina kategoria ya kihusishi na kile ambacho wengine wanakiita kihusishi wamekijumuisha ndani ya kategoria kiunganishi ambayo akina Khamisi na Kiango wanayo pia. Aidha Kihore na wenzake wanakiri kuwepo kwa uhusishi kama kategoria ndogo ndani ya kategoria kuu ya kiunganishi. Tofauti nyingine inayojitokeza hapa ni ya kiitikisadi tu. Khamisi na Kiango wanapenda kufupisha istilahi ilihali wenzao huridhika zikiwa ndefu. Kutokuwepo kwa istilahi zilizosanifiwa na kukubalika na wanaisimu wa isimu ya Kiswahili iliyofundishwa kwa zaidi ya miaka 25, kunaonekana kuwa ni mgogoro unaohitaji utatuzi. Mukuthuria (2000)·anaiita hali hii kuwa ni mtafaruku wa istilahi za Kiswahili.

Bila shaka kuzuka kwa istilahi mpya kwa dhana ambazo tayari zina msamiati wa kuziwakilisha ni ishara kuwa istilahi zilizoundwa hazikubaliki kwa watumiaji wote hali hii inashadidiwa na Musau na Onyango (2000:2) wanapokiri.

> *Kwa kipindi cha miaka ishirini hivi, kozi za msingi za isimu nchini Kenya zimekuwa zikifundishwa kwa Kiswhaili. Kozi hizo zimeundiwa istilahi mwafaka za kufundishia ingawa hakuna ukubaliano miongoni mwa walimu wanaofundisha isimu katika vyuo mbalimbali kuhusiana na istilahi zinazotumiwa.*

Kutokuwapo na mwafaka miongoni mwa wanaisimu wa Kiswahili ni jambo ambalo ni dhahiri kama dondoo lililonukuliwa hapo juu na mifano katika jedwali la 1 na la 2 inavyoonyesha. Kwa hali yoyote ile iwayo, ufumbuzi wa tatizo la kutoafiki istilahi zilizokwishaundwa na kutumika, sio kila mwanaisimu kuunda na kutumia istilahi zake binafsi.

Mbali na kutokubaliana na istilahi zilizoundwa, lipo pia tatizo la kutokuwepo kwa istilahi zinazotosheleza kwa viwango mbalimbali. Hali hii ndiyo inamlazimisha mhitaji wa istilahi kuunda na kutumia istilahi zake. Uundaji holela wa istilahi hausaidii mawasiliano na athari yake kwa mawasiliano ni jambo lisilohitaji maelezo. Ama kuhusu istilahi za sayansi pendwa, kutofahamika kwa istilahi zinazotumika kumekuwa ni kikwazo cha kufanikisha mawasiliano baina ya wazungumzaji.

## 6.0 Juhudi Binafsi za kuunda istilahi

Uundaji wa istilahi za fani mbalimbali kama vile isimu na fasihi umekuwa ukifanywa na watu binafsi ili kukidhi mahitaji yao bila kuwashirikisha wataalamu wengine. Hii ndio hali iliyokuwapo miaka ya 1970 na 1980 katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakati fani hizi zilipoanza kufundishwa kwa Kiswahili kabla ya vitabu au istilahi za Kiswahili kwa dhana za isimu na fasihi kuundwa. Juhudi za mtu mmoja mmoja zilifikia kilele wakati wanaisimu na wanafasihi walipokutana na kuzisanifisha istilahi zao na

kisha kuzichapa katika Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha au katika jarida ili zisambae na kuwafikia watumiaji wengi na kuwawezesha wanaisimu na wanafasihi ya Kiswahili kuweza kuwasiliana kwa ufanisi zaidi. Kwa bahati mbaya istilahi zilizoshughulikiwa hadi sasa ni istilahi za msingi tu, na hazitoshelezi kufundishia mada mbalimbali za isimu kama Musau na Onyango 2000:2 wanavyokiri:

> *Ingawa juhudi kubwa zimefanywa kuunda msamiati unaowakilisha dhana za kimsingi za isimu, kungali na pengo kubwa katika shughuli hiyo. Kuna dhana nyingi katika nadharia ya isimu ya Kiswahili ambazo hazijaundiwa msamiati wa Kiswahili*

Kutokana na upungufu huu wa istilahi wanaisimu binafsi bado wanaendelea kuunda na kutumia istilahi zao peke yao. Tazama mfano wa istilahi za Musau na Onyango walizounda kwa ajili ya dhana za msingi zinazotumika kufundisha lugha ya pili kama tunavyoona katika jedwali la 3.

**Jedwali la 3: Istilahi za isimu ya Kiswahili kwa kozi ya lugha ya pili**

| **Istilahi za Kiingereza** | **Mapendekezo ya istilahi za Kiwahili** |
|---|---|
| *accommodation* | usawazishaji wa usemi |
| *disfluency* | udodosaji |
| *learning strategy* | mkakati wa ujifunzaji |
| *simplification* | usahilishaji |
| *suggestopedia* | udokezi |
| *conditioning* | uzoeshaji |

Istilahi hizi ni mapendekezo ya Musau na Onyango ambao huzitumia wanapofundisha nadharia ya isimu katika Chuo Kikuu cha Kenyatta. Kwa kuwa istilahi hizi zilitungwa kukidhi haja yao ya kupata istilahi za kufundishia, hazifahamiki kwa walimu wengine wa somo hili katika vyuo vikuu vingine vya Afrika Mashariki. Bila shaka wahadhiri wengine wanaokabiliwa na tatizo kama hili huunda istilahi zao kwa dhana hizi kwa lengo lilelile la akina Musau na Onyango na athari yake katika mawasiliano haihitaji mjadala.

Istilahi za sayansi pendwa zimekuwa zikiundwa ili kukidhi mahitaji ya kutoa elimu kwa umma. Istilahi zilizoundwa na kusanifiwa na BAKITA zililenga kutimiza lengo hili. Jedwali la 4 ni kielelezo cha istilahi za aina hii:

**Jedwali la 4: Istilahi za Sayansi pendwa**

| Msamiati wa Kiingereza | Msamiati wa Kiswahili |
|---|---|
| *malnutrition* | utapiamlo |
| *marasmus* | nyongea |
| *nutrients* | virutubisho |
| *parasite* | vimelea |
| *acid* | asidi |
| *glucose* | glukozi |

Wakati mwingine uundaji wa istilahi ulifanywa kwa dharura na watu binafsi ili kukidhi haja ya kuwa na istilahi za kuwakilisha dhana iliyohitaji neno la Kiswahili. Hali hii hutokea wakati mkalimani au mfasiri anapotakiwa kutafsiri matini ya kisayansi ambayo ina dhana ambazo Kiswahili hakina msamiati wa kuziwakilisha. Kutokana na haja hii mfasiri au jopo la wafasiri au waandishi huunda na kutumia istilahi ambazo nazo hazijasanifiwa wala kujulikana kwa wengine zaidi ya wao. Tazama mfano wa 1 chini:

**Mfano wa 1**.

mshika dau - *stake holder*
bioanuwai - *biodiversity*

Msamiati wa sayansi pendwa unapotumiwa katika hadhara yoyote ile iwayo, iwe ni mhadhara, hotuba n.k. huwatatiza wasikilizaji na kuwafanya washindwe kuelewa kile kinachoelezwa ikizingatiwa kuwa wasikilizaji sio wanafunzi ambao huweza kurejelea kamusi zao au kumwuliza mtoa mada awaeleze maana ya istilahi iliyotumika. Katika mazingira haya msikilizaji atalazimika kujaribu kudodosa maana ya neno kutokana na muktadha lilipotumika. Kwa hali hii mawasiliano huwa yanatatizika na kuathirika.

## 7.0 Mambo ya kuzingatia ili istilahi zifanikishe mawasiliano

Istilahi zinazotumika katika Kiswahili kueleza dhana za fani mbalimbali kama vile afya, uchumi, lishe, ufundi na biashara na hata kwa elimu ya msingi huwa ngeni sana kwa watu wasio wa fani hizo ambao ama kwa sababu hawaijui lugha hiyo kwa kuwa walipata elimu yao kwa Kiingereza zamani, au hawajawahi kuipata elimu hiyo kabisa. Tazama mfano wa 2 chini:

**Mfano wa 2:**

Utapiamlo, nyongea, virutubisho, kimelea, virusi, mtindio wa ubongo, mshika dau, bioanuwai

Lugha ya Kiswahili inapotumiwa kueleza maarifa ya kawaida ambayo kwa muda mrefu yamekuwa yakielezwa kwa Kiingereza, Waswahili wasioielewa lugha ya taaluma hii

hulalamika kuwa Kiswahili kinakuwa kigumu. Na iwapo walalamikaji wana mtazamo hasi dhidi ya Kiswahili kuchukua dhima ya kuwa lugha ya kufundishia katika viwango vyote vya elimu, hudai kuwa Kiswahili kinafanywa kigumu kwa makusudi, na kwamba Kiswahili ni kigumu kiasi kwamba wanalazimika kutumia kamusi wanaposoma matini za Kiswahili ili kuelewa maana za baadhi ya maneno wanayoyasoma katika matini. Kwa kuwa wanaamini kuwa wana umahiri wa kutosha wa lugha hii, hawaelewi kwa nini Kiswahili kinakua kigumu kiasi cha wao kushindwa kuelewa jambo lililoandikwa kwa Kiswahili. Hoja kama hizi zinapotolewa na wasomi (ambao ndio wanatatizika zaidi kuliko wazungumzaji wa kawaida), maswali kadha huibuka: Je Kiswahili ni kigumu au kinafanywa kigumu? Hoja za Kiswahili kuwa kigumu zinatolewa na wale wasiokubali au kufahamu kuwa lugha ya kitaalamu ni lugha ya peke yake ambayo mtu lazima ajifunze. Hizi ni hoja za wale wanaofikiri wanafahamu Kiswahili, wasijue kuwa wanachofahamu ni Kiswahili cha kawaida kinachotumiwa katika mawasiliano ya kila siku mitaani, ofisini au katika majukwaa ya siasa.

Matumizi ya istilahi yanaweza kufanikisha mawasiliano iwapo lugha ya taaluma itafahamika. Ni muhimu kwa kila mzungumzaji wa Kiswahili kutambua kuwa kila fani ina lugha yake ambayo ni lazima kuijua na asiyeijua hatoelewa kitakachoelezwa katika lugha hiyo. Ili lugha ya taaluma ifahamike, mambo kadha hayana budi kuzingatiwa. Hapa tutajadili mambo manne: haja ya kujifunza Kiswahili cha kitaalamu, umuhimu wa Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia, haja ya kuunda na kusanifisha istilahi za kutosha kwa kila kiwango na kwa nyanja zote, na umuhimu wa kusambaza istilahi kwa watumiaji wake wote ili wazijue na kuzitumia.

## 7.1 Kujifunza Kiswahili cha kitaalamu

Kiswahili cha kitaalamu ni tofauti na Kiswahili cha kawaida kizungumzwacho mitaani. Kiswahili cha kitaalamu kama lugha nyingine ina msamiati wake, na atakaye kuijua hana budi kujifunza. Kiswahili cha kitaalamu, hueleweka kwa wale ambao wanajishughulisha na taaluma hiyo. Kwa kuwa Kiswahili ndio kwanza kinaanza kukua, msamiati wa sayansi pendwa na sayansi menyu utaingia kwenye lugha hii. Kwa walio wengi ambao hawasomi matini zenye msamiati huu, huenda Kiswahili hiki kipya kikawatatiza.

Istilahi za fani mbalimbali huingia katika Kiswahili na Waswahili hukutana nazo wanaposoma vitabu, magazeti, ripoti za semina au hotuba za viongozi zinazozungumzia masuala mahsusi kama vile uchumi, afya ya jamii, lishe, biashara n.k. kwa hali hii ni dhahiri kuwa Kiswahili kitaendelea kupata msamiati wa fani mbalimbali kadri dhana mpya zinavyoingia katika lugha hii. Kwa hivyo Waswahili hawana budi kujifunza na kuzitumia istilahi za Kiswahili ambazo sio mahsusi tena kwa wataalamu wa fani hizo, lakini bado hazijawa msamiati wa kawaida. Lakini ili kufanikisha matumizi ya istilahi mbalimbali katika Kiswahili, lugha hii inapaswa kuwa lugha ya mawasiliano katika elimu.

## 7.2 Kiswahili kiwe lugha ya mawasiliano katika nyanja zote za elimu

Wazungumzaji wa Kiswahili wataweza kufahamu lugha ya kitaalamu hasa kwa sayansi pendwa ambayo kwa kiasi kikubwa inaenea kwa jamii nzima kupitia vitabu na majarida mbalimbali, vyombo vya kupashana habari kama vile magazeti, radio na televisheni iwapo Kiswahili kitakuwa lugha ya mawasiliano kwa jamii nzima katika nyanja zote za elimu. Mambo kadha yamekuwa ni kikwazo kwa Kiswahili cha kitaaluma hususan cha sayansi pendwa kukua na kuenea. Tatizo kubwa ni kwa Kiswahili kutopewa fursa ya kukua na wale wenye mamlaka ya kisiasa au ushawishi wa kisomi. Wasomi na watawala hupendelea kudumisha hali iliyopo ambapo kundi dogo la watu katika jamii wanaojua Kiingereza linahodhi taaluma ambayo hupatikana kwa wale wanaoifahamu lugha hii ya kigeni. Ili kudumisha hali hii hupinga juhudi za kutumia Kiswahili kuwa lugha ya elimu. Sera ya kutumia Kiswahili kama lugha ya taaluma ama inapingwa na iwapo imekwishatungwa haitekelezwi kwa sababu itaongeza ushindani katika kupata maslahi ya jamii na hivyo kuwapunguzia fursa za kupata upendeleo wale wachache wanaofaidi. Kutokana na hisia hizi hasi, Kiswahili hupondwa kuwa hakiwezi kueleza sayansi na teknolojia kama kifanyavyo Kiingereza kwa sababu sio lugha ya sayansi na kwamba hata wazungumzaji wake hawana teknolojia yao wenyewe.

## 7.3 Kuunda na Kusanifisha istilahi za kutosha

Juhudi za kuunda istilahi za Kiswahili kwa fani mbalimbali zimekuwa zikifanywa kwa miaka mingi sasa na orodha kadha za istilahi zimeandikwa, kama vile *Tafsiri Sanifu za BAKITA Kitabu cha 1 - 5* na *Tafsiri Sanifu za Hisabati*. Aidha zimetungwa pia kamusi kadha za fani tofauti: Sheria, Ubaharia Wanyama na nyoka, Ufundi, Magonjwa ya mimea, mifugo, na wadudu waharibifu, Sayansi na Teknolojia, Isimu na lugha, Fizikia, Kemia na Biolojia, Biashara n.k. Istilahi hizi bado ni chache. Tunaweza kukiri kuwa karibu kila fani ina msamiati japokuwa ni kwa kiwango cha elimu ya msingi au sekondari tu. Ipo haja kuunda istilahi zaidi zitakazokidhi haja ya masomo ya kiwango cha chuo kikuu. Uundaji wa istilahi lazima uzingatie sifa bainifu za istilahi bora kama zilivyoorodheshwa na Felber (1984) na kunukuliwa na Mwansoko (1998:32). Sifa hizo ni pamoja na istilahi kuwa:

(a) sahihi, (b) fupi, (c) rahisi kutamka (d) rahisi kunyambulika ili kuunda istilahi kikoa,

(e) inazingatia sarufi ya lugha lengwa (f) inawakilisha dhana moja tu na

(g) inakuwa katika mfumo wa kidhana.

Umuhimu wa istilahi kuwa na sifa hizi ni kwamba zinakuwa rahisi kueleweka kumwezesha mtumiaji kujenga taswira ya dhana inayowakilishwa. Aidha istilahi zenye sifa hizi hupata hukubaliwa na watumiaji wengi kwa urahisi. Kinyume chake ni kwamba watumiaji ambao hawataziafiki istilahi zilizoundwa, huweza kuunda zao na jambo hili likitokea huweza kuathiri mawasiliano kutokana na dhana moja kuwakilishwa na istilahi zaidi ya moja. Matumizi ya istilahi tofauti kwa dhana moja huwakanganya watumiaji. Mifano ya istilahi katika jedwali 1 kama zilivyonukuliwa na Mwansoko (1995) ni kielelezo cha matokeo ya istilahi zisizokubalika.

## 7.4 Kusambaza istilahi zilizoundwa

Istilahi nyingi za Kiswahili zimeundwa na BAKITA na TUKI au watu binafsi na kusanifishwa na BAKITA. Taasisi zote hizi zipo Tanzania. Halikadhalika walimu wa fasihi na isimu katika vyuo vikuu vya Kenya na Tanzania nao huunda istilahi kwa ajili ya matumizi yao. Kazi hizi hazifahamiki sana kwa wale ambao hawakuhusika kuziunda kwa sababu hapana mfumo ulio bayana wa kusambaza istilahi za Kiswahili miongoni mwa wanazuoni wa Afrika ya Mashariki wanaojishughulisha na taaluma mbalimbali kwa Kiswahili. Kwa hali hii baadhi ya watumiaji ama hawazijui au hawazipendi na badala yake hutunga istilahi zao kwa dhana ambazo tayari zina istilahi. Mfano wa istilahi za isimu uliojadiliwa katika jedwali 1 ni kielelezo tosha. Kwa hali hii basi ingefaa utaratibu ubuniwe wa kusambaza istilahi kila mara ili kuepuka kuzirudufu. Ingefaa taasisi za Kiswahili za Afrika Mashariki zikawa na mtandao wao (*webpage*) katika kompyuta ambamo istilahi zingeingizwa kwa kila mmoja kusoma na kutoa maoni na kisha kuamua istilahi itakayosadifu kutumiwa.

## 7.5 Kuandika machapisho ya kitaalamu kwa Kiswahili

Idadi ya aina za fani zenye istilahi za Kiswahili hazioani na machapisho ya Kiswahili kwa fani hizo. Mbali na taaluma ya isimu na fasihi, na siku hizi historia (baada ya majuzuu manane ya historia kuu ya Afrika kutafsiriwa na UNESCO chini ya uratibu wa TUKI), taaluma nyingi hazijaandikwa sana katika Kiswahili. Matini za kitaaluma zitawachochea Waswahili kusoma maarifa haya na kujifunza msamiati wake. Bila shaka ukosefu wa motisha wa kuandika kwa Kiswahili ndio wenye kusababisha hali hii. Laiti sera za lugha za nchi zetu zingekuwa zinapenda Kiswahili kuwa lugha ya taaluma hali hii ingebadilika. Kwa vile uandishi ni kazi kubwa, huenda ingefaa jitihada

za kufasiri vitabu kama ilivyofanywa kwa historia kuu ya Afrika zingefanywa ili kuwapatia watu wetu machapisho mengi ya kitaaluma kwa Kiswahili.

## 8.0 Hitimisho

Makala imechunguza na kuonyesha kuwa matumizi ya istilahi huweza kuathiri mawasiliano kwa walei na wanataaluma pia. Tatizo kwa wanataaluma ni kubwa zaidi itokeapo istilahi zaidi ya moja hutumiwa na wanazuoni tofauti kuwakilisha dhana moja. Katika hali hii imependekezwa kuwa juhudi hazina budi kufanywa kusanifisha istilahi, na kuandika kwa Kiswahili vitabu katika taaluma mbalimbali ili kupata matini nyingi za Kiswahili ambazo sio tu kwamba zitasaidia kuelimisha jamii katika lugha wanayoijua, bali kuufanya msamiati wa taaluma mbalimbali kuenea na kufahamika pia.

## MAREJEO


Alberts, M. R. (1999). Terminology in South Africa. LEXIKOS Vol. No. 9. Buro die WAT, Stellenbosch.

Feber, H. (1984). *Terminology Manual*. Paris, Infoterm/UNISIST/UNESCO.

Massamba, D. P. (1996). Problems in Terminology Development: The Case of Tanzania. KISWAHILI Vol. No.59. TUKI, Dar es Salaam.

Mukuthuria, M. (2000). Uhakiki wa Mtafaruku wa Istilahi za Kiisimu na Nafasi ya Usawazishaji katika Maendeleo ya Kiswahili. Makala iliyosomwa katika Kongamano la Kiswahili kwa Matumizi Maalum. Mombasa 2 - 6 Oktoba, 2000. Haijachapishwa.

Musau, P. M. na Jakton O. Onyango (2000). Uundaji wa Istilahi za Kiisimu: Mapendekezo katika kozi ya Lugha ya Pili. Makala iliyosomwa katika kongamano la Kiswahili kwa Matumizi Maalum. Mombasa 2 - 6 Oktoba 2000. Haijachapishwa.

Mwansoko, H. J. M. (1995). Uundaji wa Istilahi za Kisiasa Tanzania. KIOO CHA LUGHA Juzuu 1 & 2. Jarida la Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar esSalaam.

Mwansoko, H. J. M. (1998). Nidhamu katika Utumiaji wa Istilahi za Kiswahili: Mifano kutoka fani ya Isimu. MULIKA Juzuu Na. 24. TUKI, Dar es Salaam.

Temu, C. W. (1984). Kiswahili Terminology: Principles adopted for the Enrichment of Kiswahili Language. KISWAHILI Journal Vol. No. 51/2. TUKI, Dar es Salaam.